**HOTUBA YA MGENI RASMI KATIBU MKUU KIONGOZI WA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA BALOZI MHANDISI JOHN W.H. KIJAZI (KWA NIABA YA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHESHIMIWA DKT. JOHN POMBE MAGUFULI) KWENYE HAFLA YA UZINDUZI WA KIVUKO CHA MV. RUBONDO ISLAND NA UTALII WA SOKWE KATIKA HIFADHI YA TAIFA YA KISIWA CHA RUBONDO – HAFLA ILIYOFANYIKA ENEO LA KASENDA, WILAYA YA CHATO, MKOANI GEITA TAREHE 22 JUNI, 2020**

---

*Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Mbunge wa Chato, Dkt. Medard Kalemani;*

*Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa ya Geita, Kagera na Mwanza;*

*Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu;*

*Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Geita pamoja na Wenyeviti wa CCM wa Wilaya mliopo;*

*Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali mliohudhuria;*

*Makatibu Tawala wa Mikoa ya Geita, Kagera na Mwanza;*

*Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya TANAPA, Jenerali George Waitara, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi ya Tanzania Mstaafu;*

*Wenyeviti wa Bodi za Wakala wa Misitu (TFS) na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC);*

*Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya za Chato, Geita, Nyang'wale, Bukombe na Mbogwe; pamoja na Wakuu wa Wilaya nyingine toka Mikoa ya Mwanza na Kagera.*

*Mwakilishi wa Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT);*

*Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini ya TANAPA;*

*Wajumbe wa Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa ya Geita, Kagera na Mwanza;*

*Kamishna wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Dkt. Allan Kijazi, na Makamishna wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS);*

*Wajumbe wa Bodi na Menejimenti ya Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC);*

*Wawakilishi toka Chama cha Waendesha Shughuli za Utalii Tanzania (Tanzania Association of Tour Operators - TATO), Shirikisho la Vyama vya Waendesha Utalii Tanzania (Tourism Confederation of Tanzania - TCT), na Chama cha Wamiliki wa Hoteli za Kitalii Tanzania (Hotels Association of Tanzania - HAT) mliopo hapa;*

*Makamishna Wasaidizi, Askari wa Jeshi Usu na Watumishi wote wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania mliopo hapa;*

*Viongozi wa Dini zote na wa Vyama vya Siasa mliopo hapa;*

*Viongozi na Watendaji wote wa Serikali mliopo hapa;*

*Waandishi wa Vyombo mbalimbali vya Habari mliohudhuria shughuli hii;*

*Wananchi wote na Wageni waalikwa mliohudhuria;*

*Mabibi na Mabwana.*

**Habari ya mchana.**

Napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na fadhila, kwa kutujalia na kutuwezesha sisi sote kujumuika mahali hapa siku ya leo kwa ajili ya kufanikisha tukio hili muhimu.

Aidha, napenda kipekee kabisa kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa kunipa heshima ya kumuwakilisha kwenye tukio hili muhimu la **uzinduzi wa Kivuko cha 'MV. Rubondo Island',** pamoja na **kuzindua utalii wa wanyama adimu aina ya Sokwemtu** kwenye Hifadhi ya Kisiwa cha Rubondo.

***Ndugu Wananchi na Viongozi mliohudhuria;***

Nawasilisha kwenu salamu nyingi kutoka kwa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli na amenituma niwahakikishie kuwa amefurahishwa na kuridhishwa na kazi nzuri iliyofanywa na wahusika wote hadi kufanikisha tukio hili muhimu linalofanyika leo, ambalo ni moja ya hatua muhimu katika kuleta maendeleo kwa wananchi wa Ukanda huu wa Ziwa, na kwa Taifa letu kwa ujumla kupitia Sekta ya Utalii. Mheshimiwa Rais alitamani sana kushiriki nanyi kwenye tukio hili la kihistoria, lakini kutokana na majukumu mengine ya Kitaifa yanayomkabili ameshindwa kuhudhuria hapa leo.

***Ndugu Wananchi, Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Kabla sijazungumzia tukio hili lililotuleta hapa leo, napenda kwanza nizungumzie Sekta ya Utalii kwa ujumla wake ili kuonyesha umuhimu wa Sekta hii kwa nchi yetu, pamoja na jitihada za Serikali katika kuiendeleza sekta hii.

Kwanza napenda kutoa pongezi za dhati kwa Wizara ya Maliasili na Utalii, Bodi ya Wadhamini ya TANAPA, Uongozi wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori kwa ujumla, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhifadhi rasilimali za wanyamapori hapa nchini. Kazi inayotekelezwa na Wizara pamoja na Taasisi zake nilizozitaja imeiletea heshima na mafanikio nchi yetu katika Sekta ya Utalii. Katika kipindi cha Serikali hii ya Awamu ya Tano, tumeshuhudia kuongezeka kwa idadi ya watalii mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, idadi ya wageni wanaokuja nchini kwetu kwa shughuli za utalii imeongezeka kutoka wageni **1,137,182** mwaka **2015/2016** hadi kufikia wageni **1,527,230** mwaka **2018/2019** ambalo ni ongezeko la asilimia 34.3 (34.3%) huku wastani wa siku wageni hao walizokaa nchini kwetu zikiongezeka toka **siku 10** katika mwaka **2015/2016** kufikia **siku 13** katika mwaka **2018/2019**. Malengo ya Serikali ni kufikia watalii **milioni 2.5** kwa mwaka ifikapo mwaka **2024/2025**. Ongezeko hilo la watalii

litaongeza mchango wa Sekta ya Utalii katika Pato la Taifa (GDP) kutoka **asilimia 17** inayochangia sasa, hadi kufikia **asilimia 19.5** mwaka **2024/2025**.

*Ndugu Wananchi na Wageni waalikwa;*

Ili kufikisha lengo la watalii **milioni 2.5** kwa mwaka ifikapo mwaka **2024/2025**, Serikali ya Awamu ya Tano imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kufanikisha azma hiyo. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na kufufua Kampuni yetu ya Taifa ya Ndege (**ATCL**) kwa kununua ndege mpya kumi na moja (**11**). Kati ya ndege hizo mpya kumi na moja zilizonunuliwa na Serikali, tayari ndege nane (8) zilikwishawasili nchini na zinatumiwa na Kampuni yetu ya Taifa ya Ndege kutoa huduma za usafiri ndani na nje ya nchi. Ndege tatu (3) zilizobaki ambazo hazijawasili nchini zinatarajiwa kufika mwishoni mwa mwaka huu wa 2020 na katikati ya mwaka 2021.

Hatua nyingine ambazo Serikali imechukua ni pamoja na:

- Kujenga viwanja vipya vya ndege,
- Kuvifanyia ukarabati viwanja vya ndege vilivyopo,
- Kujenga Jengo la Tatu la Abiria (Terminal 3) kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere (JNIA) uliopo Dar es Salaam,

- Kufanya upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Jijini Mwanza,
- Kuboresha miundombinu ya barabara kwenda kwenye vivutio mbalimbali vya utalii nchini, na
- Kuanzisha Chaneli Maalum ya Utalii katika Televisheni ya Taifa (TBC) ijulikanayo kama "*Tanzania Safari Channel*" kwa ajili ya kuvitangaza vivutio vyetu mbalimbali vya utalii kitaifa na kimataifa.

Lakini pia katika hatua nyingine ya kuimarisha utalii wetu na kuongeza idadi ya watalii, Serikali imeyapandisha hadhi baadhi ya yaliyokuwa Mapori ya Akiba kuwa na hadhi ya Hifadhi za Taifa, na hivyo kufanya Hifadhi zetu za Taifa kuongezeka na kufikia idadi ya **22** mwaka 2020 toka idadi ya Hifadhi za Taifa **16** zilizokuwepo mwaka 2015 kama nitakavyofafanua hivi punde.

***Ndugu Wananchi na Wageni Waalikwa;***

Serikali imeamua kuongeza wigo wa utalii kwa kuanzisha Mtandao Mpya wa Utalii (*Tourist Circuit*) wa **Kanda ya Ziwa** (*Lake Zone Tourist Circuit*) na ule wa **Kanda ya Kusini** (*Southern Tourist Circuit*) ambao kitovu chake kiko Mkoani Iringa. Kanda hizi zinalenga kuongeza vivutio vya utalii, na kuongeza fursa za

uwekezaji katika Utalii kutokana na Maliasili zilizopo kwenye maeneo haya, ambayo katika siku za nyuma utalii wake ulikuwa mdogo.

Kwa upande wa Mtandao wa Utalii wa Kanda ya Ziwa, Serikali imeanzisha **Hifadhi za Taifa mpya tatu** za **Burigi-Chato**, **Ibanda Kyerwa** na **Rumanyika-Karagwe**, hivyo kufanya mtandao wa Utalii katika Kanda ya Ziwa sasa kuwa na jumla ya Hifadhi za Taifa sita (6) ikiwemo Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Rubondo, Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Saanane, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti pamoja na Hifadhi hizi mpya tatu nilizozitaja.

Serikali pia imejenga uwanja mpya wa Ndege wa Kimataifa wa Chato (*Chato International Airport*) ili kurahisisha usafiri wa watalii toka maeneo mbalimbali nchini na nje ya nchi, ikiwa ni pamoja na kuwezesha Watalii kutoka katika nchi jirani za Burundi, Rwanda, Kenya na Uganda kuweza kuvifikia vivutio hivi kwa urahisi zaidi.

Kama nilivyosema awali, kwa ujumla hatua zote hizi zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ya Awamu ya Tano zina lengo la kukuza uchumi wa nchi yetu kupitia Sekta ya Utalii, kwani kukua kwa uchumi kutaiwezesha Serikali kutoa huduma nyingi na bora zaidi kwa wananchi wake.

Lakini pia kuongezeka kwa shughuli za utalii **kutawapatia fursa wananchi wa maeneo husika kuongeza kipato chao** kupitia shughuli mbalimbali za **kuuza bidhaa ama kutoa huduma mbalimbali kwa watalii** wanaotembelea vivutio vilivyopo katika maeneo mbalimbali nchini, ikiwa ni pamoja na Vivutio vya ukanda wenu huu wa Ziwa.

***Ndugu Wananchi na Wageni waalikwa;***

Baada ya maelezo haya ya jumla ya utangulizi, sasa naomba nizungumzie tukio hili muhimu lililotuleta hapa. Leo tumekusanyika hapa ili kushuhudia tukio hili muhimu la kihistoria, ambalo pamoja na kukuza Mtandao wa Utalii katika Kanda ya Ziwa, lakini pia litaimarisha huduma za usafiri wa majini na ulinzi wa rasilimali zetu katika Ziwa Victoria.

Napenda niwakumbushe tena kuwa uzinduzi wa kivuko hiki leo ni utekelezaji wa ahadi aliyoitoa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli mnamo tarehe 31 mwezi Desemba mwaka 2019 alipotembelea Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Rubondo.

Kivuko hiki, licha ya kuondoa adha ya usafiri kwa watalii, kitawezesha pia watalii kutoka Kisiwani Rubondo kwenda Hifadhi Jirani ya Burigi-Chato, Kisiwa

cha Saanane na eneo la Ghuba ya "Speke" iliyopo karibu na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Kwa maana hiyo, kuwepo kwa Kivuko hiki kutawezesha wageni kufanya utalii wa **majini**, wa **kisiwani** na wa **nchi kavu**, na hivyo basi kupanua wigo wa utalii katika ukanda huu wa Ziwa.

***Ndugu Wananchi na Wageni Waalikwa***;

Sambamba na kuzindua kivuko cha "MV Rubondo Island", leo pia nitazindua Utalii wa Sokwemtu (Chimpanzee) katika Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Rubondo. Hapa Tanzania Utalii wa Sokwemtu ulikuwa ukifanyika kwenye Hifadhi za Taifa za Gombe na Mahale pekee. Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Rubondo sasa inakuwa ni Hifadhi ya Taifa ya **tatu** hapa nchini ambapo utalii wa Sokwemtu unafanyika. Hivyo, Watalii wanaotoka katika Hifadhi nyingine maarufu Duniani kama vile Hifadhi ya Taifa ya Serengeti iliyopo Tanzania, na wale wanaotoka nchi za jirani za Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi, sasa watapata fursa ya kufanya utalii wa Sokwemtu katika Kisiwa cha Rubondo, pamoja na Utalii wa Uvuvi, yaani "Sport Fishing".

Kama ambavyo mmejulishwa awali, Sokwemtu wa Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Rubondo ni wa kipekee, kwani asili yao ni kutoka Afrika Magharibi, ambapo walichukuliwa na kupelekwa kwenye bustani ya Wanyama huko Ulaya, na

baadaye kuletwa kwenye mazingira yetu ya asili katika Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Rubondo. Kupitia hafla hii, napenda kuchukua nafasi hii kuwakaribisha watalii kutoka sehemu mbalimbali nchini na duniani kote kwa ujumla, kuja kutembelea na kuona Wanyama hawa adimu.

***Ndugu Wananchi na Wageni Waalikwa;***

Ili kufanikisha shughuli zetu za utalii hapa nchini, ni muhimu sana kwa Serikali kuishirikisha kikamilifu Sekta Binafsi. Hivyo basi, napenda kutoa wito kwa **wawekezaji** wa Sekta ya Utalii kutoka sehemu mbalimbali nchini na nje ya nchi kutembelea Ukanda huu mpya wa Utalii wa Kanda ya Ziwa ili kuziona na kuzitambua fursa nyingi za uwekezaji zilizopo kwenye sekta ya utalii kama vile huduma za **malazi**, **usafirishaji** na **chakula** na kuzitumia fursa hizi kwa kufanya uwekezaji unaohitajika. Serikali inawahakikishia Wawekezaji kuwa itawaunga mkono na kuwawekea mazingira rafiki na wezeshi katika uwekezaji wao huo, kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.

Kipekee, napenda kutoa wito kwa wananchi wanaoishi katika Ukanda huu wa Ziwa wa Utalii kuchangamkia fursa mbalimbali nilizozitaja ikiwa ni pamoja na kuuza bidhaa mbalimbali na kutoa huduma mbalimbali zinazohitajika kwa

Watalii zilizo ndani ya uwezo wenu. Msipochangamkia fursa hizi, basi mjue watakuja watu wengine kutoka nje ya Kanda ya Ziwa na kuzichukua fursa hizo.

***Ndugu Wananchi na wageni waalikwa;***

Kabla ya kumaliza hotuba yangu, napenda kwa mara nyingine kuipongeza sana Bodi ya Wadhamini ya TANAPA chini ya Mwenyekiti wake Jenerali (Mstaafu) George Waitara, pamoja na Menejimenti ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) kwa kazi nzuri sana mnayoifanya, ikiwa ni pamoja na kutekeleza miradi ya kimkakati ikiwemo ujenzi wa Hoteli ya Nyota tatu (*Burigi Chato Hotel*) yenye jumla ya vitanda **50** kwa ajili ya kupunguza changamoto ya malazi kwa watalii katika ukanda huu. Endeleeni na utendaji huu mzuri wenye tija kubwa kwa nchi yetu na hongereni sana.

Napenda pia kuwapongeza Wizara ya Maliasili na Utalii na mamlaka mbalimbali zote za uhifadhi nchini kwa kazi kubwa mnayofanya ya kudhibiti vitendo vya ujangili nchini, kwani kwa sehemu kubwa ujangili sasa umepungua. Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli inatambua kazi kubwa mnayoifanya. Katika kuongeza mapambano dhidi ya vitendo vya ujangili, ndio maana Serikali ya Awamu ya Tano imeamua kuanzisha Jeshi Usu la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu yetu (*Wildlife and*

*Forest Conservation Service*) linalosimamia maeneo yote yaliyohifadhiwa nchini. Tayari Marekebisho ya Sheria husika (*Written Laws* (*Miscellaneous Amendments*) *Act 2020*) yamefanyika na kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivi karibuni, na tayari Mheshimiwa Rais amesaini marekebisho hayo ya Sheria. Hivyo, sasa Jeshi Usu la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu ambalo lipo rasmi kwa mujibu wa Sheria liendelee kutekeleza wajibu wake kikamilifu.

Napenda pia kuipongeza Kampuni ya Kitanzania ya *M/S Songoro Marine Ltd* kwa kazi nzuri waliyofanya ya kukitengeneza Kivuko hiki cha "MV. Rubondo Island". Hongereni sana na endeleeni na utendaji mzuri katika kazi nyingine ambazo Serikali itawapatia katika siku zijazo. Serikali siku zote inatoa kipaumbele kwa Kampuni za ndani pale inapodhihirika kuwa zinao uwezo wa kutekeleza kazi husika na gharama zao ni nafuu zaidi kuliko za Makampuni ya Nje. Hongereni sana Kampuni ya M/S Songoro Marine Ltd.

Navipongeza pia vikundi vyote vya Burudani vilivyoshiriki katika shughuli hii na kuifanya ifane sana kwa burudani nzuri mliyotoa. Hongereni sana.

Navishukuru pia vyombo vyote vya habari vilivyoshiriki katika kuwahabarisha wananchi juu ya tukio hili. Nawashukuru kwa ushirikiano wenu.

Mwisho kabisa ila sio kwa umuhimu, napenda kutoa wito kwa wananchi kuendelea kuheshimu mipaka ya Hifadhi zetu za Taifa na maeneo mengine yaliyohifadhiwa nchini, na kushiriki kikamilifu katika kuzilinda rasilimali zetu ili tuendelee kupata manufaa ya kiutalii kwa faida ya kizazi kilichopo na vizazi vyetu vijavyo.

***Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana***;

Baada ya maelezo haya, sasa ninayo furaha kutamka kuwa Kivuko cha MV RUBONDO ISLAND na Utalii wa SOKWEMTU katika Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Rubondo VIMEZINDULIWA RASMI.

Mungu Ibariki Afrika
Mungu Ibariki Tanzania
**Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.**